



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAULI YA WILAYA YA ITILIMA

SHULE YA SEKONDARI IKUNGULIPU



S.L.P 259 BARIADI-SIMIYU-0785295946/0763276723

Ikungulipusecondary2020@gmail.com

FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA

(JOING INSTRUCTION)

JINA LA MWANAFUNZI

.....

- Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari IKUNGULIPU, shule ipo katika kata ya luguru kijiji cha ikungulipu.
- Shule inafundisha masomo ya
CIVICS,HISTORY,GEOGRAPHY,KISWAHILI,BASIC MATHEMATICS,CHEMISTRY,BIOLOGY,ENGLISH LANGUAGE,PHYSICS na ICS(INFORMATION COMPUTER STUDIES)
- Masomo yote yanayofundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.
- Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11 January 2021, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo.

MAMBO YA KUZINGATIA:

SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

- 0.1:** Suruali mbili moja rangi ya kijani mgomba na nyingine rangi ya moto zenye marinda na mikunjo ya chini (turn up).
- 0.2:** Atakaye shona suruali isiyokuwa na maadili na chini ya kiwango kinachotakiwa hataruhusiwa kuvaa shuleni.
- 0.3:** Shati jeupe (nyeupe) mikono mifupi ,soksi jozi mbili rangi nyeusi

0.4: Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vyenye kamba na visiwe na visigino virefu.

0.5: Mkanda wa suruali mweusi –belt ndogo, vifaa vya michezo traki suti(nyeusi), na fulana ya damu ya mzee za mazoezi na shughuli ya kujitegemea(EK)- ZINAPATIKANA MADUKANI.

B: WASICHANA

- ✓ Sketi mbili, rangi mbili ya kijani na nyingine rangi ya moto zenye rinda kubwa. Atakaye shona sketi isiyokuwa na maadili na chini ya kiwango kinachotakiwa hataruhusiwa kuivaa shuleni.
- ✓ Shati (nyeupe) mikono mifupi, soksi jozi mbili rangi nyeupe zisizo na mapambo ya aina yoyote .
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili na visiwe na kisigino kirefu.
- ✓ Vifaa vya michezo traki rangi nyeusi na fulana za rangi ya damu ya mzee za mazoezi na shughuli za elimu ya kujitegemea(EK) –ZINAPATIKANA MADUKANI.

C: WOTE

- Daftari kubwa kumi (**COUNTER BOOKS**), mathematic set moja, dictionary ya kiingereza na kamusi ya Kiswahili.
- Sweta la rangi ya bluu(yanapatikana madukani)

N:B vazi la hijabu (kwa wale waislamu – wasichana) lifanane na sare za shule:

- Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu ambazo zitajazwa kikamilifu na kuzikabidhi wakati wa kusajiliwa shuleni.
- Kwa Yule tu aliye na matatizo ya kiafya aje na cheti cha daktari kwa uthibitisho ili atambulike shuleni
- Sheria na kanuni za shule zisomwe na kuzingatiwa na kila mwanafunzi .

HONGERA SANA,

KARIBU SHULE YA SEKONDARI IKUNGULIPU.



KABULULE C.B
THE HEAD OF SCHOOL
IKUNGULIPU SEC.
ITILIMA

NAKALA:

DSEO – ITILIMA,

